
# JARIDA MAALUM

**WIZARA YA NISHATI**

T - 01 Nov **2025**

# KARIBUNI NISHATI



WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**

Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**

Dkt. James Mataragio

**MHARIRI**

Neema Chalila Mbuja
Teresia Mhagama

**WAANDISHI**

Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Felista Charles
Petro Mwanda
Judith Hasani

**WAPIGA PICHA**

Henry Kilasila
Godfrey Mwemezi
Ruben Richard
Amanzi Kimonjo

**MSANIFU KURASA**

Brian Mbaga


© NISHATI 2025

# HONGERA

## MHE. DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI


Kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Waziri wa Nishati



# HONGERA

## MHE. SALOME WYCLIFE MAKAMBA

Kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Naibu Waziri wa Nishati



# MHE. NDEJEMBI ASISITIZA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA SERIKALI KUFIKIA 2030

- Asema siku mia moja za Rais ni dira ya kufikia malengo
- Asisitiza ushirikiano baina ya watumishi na viongozi ndani ya Wizara ya Nishati




Kwenye picha ni Mhe. Deogratius Ndejembi Waziri wa Wizara ya Nishati akiapishwa Ikulu Chamwino Jijini Dodoma.




Kwenye picha ni Mhe. Salome Makamba Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati akiapishwa Ikulu Chamwino Jijini Dodoma.

Waziri wa Nishati Mhe. Deogratius Ndejembi amewaagiza Watumishi wa Wizara hiyo kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza Vipaumbele vya Serikali katika Sekta ya Nishati ikiwemo kufikia Megawati 8,000 ifikapo 2030.

Mhe. Ndejembi ameyasema hayo wakati akizungumza na watumishi mara baada ya kuwasili Wizara ya Nishati, Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.

Amesema watumishi wa Wizara ya Nishati ndio watendaji wakuu na wenye dhamana ya kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali yaliyowekwa yanatimia kwa kufanya kazi kwa bidii , kuwataka watumishi kuchambua kwa kina hotuba ya Mhe Rais ili kuweza kufikia vipaumbele kwa wakati na kutoa huduma bora kwa wananchi wa Tanzania.

Pia amesisitiza watumishi kutumia siku mia moja za Mhe. Rais kama kipimo na kielelezo cha kutathmini uelekeo wa malengo ya Serikali.

"Sisi kama viongozi wenu tunategemea zaidi ushirikiano kutoka kwenu ninyi wataalamu wa hapa Wizara ya Nishati ili tuweze kukamilisha Vipaumbele vya Mhe. Rais alivyoviweka katika sekta yetu kwasababu tunatakiwa tuanze kwa kukimbia na sio kutembea" amesema Mhe. Ndejembi.

Nae Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Salome Makamba amewataka watumishi kushirikiana kwa pamoja na viongozi wa Wizara hiyo ili kuendesha Sekta ya Nishati kwa pamoja, na kuongeza kuwa anatambua kwamba maswala mengi ya sekta ya Nishati yameshafanyika tayari mpaka sasa.

Amesema Serikali imeshafikisha Megawat 4,000 za kiwango cha kuzalisha Umeme, hivyo ni jukumu letu kukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea na kuongeza vyanzo vingine vya uzalishaji umeme ili kufikia megawati 8,000 ifikapo 2030.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba amewashukuru viongozi hao na amewataka watumishi wa Wizara ya Nishati kutoa ushirikiano kwa viongozi hao sambamba na kutekeleza majukumu yao kwa wakati ili kuweza kutekeleza Vipaumbele vya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ifikapo mwaka 2030.






# MATUKIO KATIKA PICHA

## MAPOKEZI YA VIONGOZI WA WIZARA YA NISHATI





Picha mbalimbali za mapokezi ya Viongozi wa Wizara ya Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi Waziri wa Wizara ya Nishati pamoja na Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati Mhe. Salome Makamba mara baada ya kuwasili Wizarani hapo, Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.










JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI / MINISTRY OF ENERGY












For more info
www.nishati.go.tz
The United Republic of Tanzania
Ministry of Energy